kweli chini, ambayo ni Neno la Mungu (Dan.8:11,12; Yn.17:17; Zab.119:142). Kwa ajili ya hayo Mungu ametoa Ujumbe wa Malaika Watatu kuwaonya walimwengu waache maasi hayo. Kama hawasikii, amewaandalia mapigo saba ya Ufunuo 16, ambayo mwisho wake yatashuhudia kuja kwa Yesu mara ya pili kuwachukua wateule wake.

Kuna sintofahamu nyingi kuhusu Injili na Sheria, Imani na Amri Kumi, Neema na Sheria. Mambo hayo mawili yanakwenda bega kwa bega. Kwa maana kama Amri Kumi hazipo, ambazo zinaonesha dhambi ni nini, basi, dhambi haiwezi kuwapo. Hivyo hatuwezi kuhitaji Injili maana hakuna dhambi; wala hatuwezi kumhitaji Mwokozi. Lakini sasa kwa kuwa Amri Kumi bado zinawafunga wanadamu, ndio maana tunahitaji Injili inayotuonesha Mwokozi awezaye kutupatia haki kwa imani peke yake.

Lakini kama Paulo asemavyo, **"Kwa maana siionei haya Injili, kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia" (Rum.1:16).** Ni kweli sheria haiokoi; hiyo siyo kazi yake. Sheria ni kioo cha kujiangalia kuona tusimamavyo mbele za Mungu, kioo hakimsafishi mtu, inabidi atafute maji na sabuni asafishwe (Yak.1:22-25; Gal.3:24).

Kioo kinahitajika, sabuni na maji vinahitajika (Sheria inahitajika, damu ya Yesu inahitajika). Wokovu hupatikana kwa neema kwa njia ya imani peke yake, lakini mtu aliyeokolewa kwa neema kwa njia ya imani lazima aoneshe matendo mema aliyoumbiwa nayo (Efe.2:8-10). Vinginevyo wokovu wake ni bure kabisa. Mwizi asiibe tena, na kadhalika. Soma Efe.4:17-32; 5:1-6; Kol.3:5-11; Gal.5:19-21; 1 Kor.6:9-11; 1 Yoh.2:4). Neema haifundishi watu kufanya maasi dhidi ya Mungu (Tit.2:11-14). Uhuru tulio nao ni wa kuchagua bwana tutakayemtumikia – Kristo au Shetani, sio kufanya tutakalo (Mt.6:24; Rum.6:15-23).

Malaika wa kwanza ana ujumbe mzito unaotangaza Injili ya milele kwa ulimwengu mzima na kuwatangazia watu kuwa hukumu inaendelea mbinguni hivi sasa wajiweke tayari na warudi kumtii Mungu aliyeumba mbingu na nchi kwa kuishika Sabato yake iliyosahauliwa (Kut.20:8-11). Sheria inayotumika katika hukumu hiyo ni zile Amri Kumi za Mungu kama zilivyotolewa mlimani Sinai (Kut.20:3-17; Yak.2:10-12). Zingatia hilo! Tunaokolewa kwa imani peke yake, lakini matendo yetu yanapimwa kwa Amri Kumi za Mungu kuona kama wokovu wetu ni wa kweli au ni maneno matupu.

**"Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji" (Ufu.14:6,7).** Mengi tumeeleza hapo juu. Kwa wanaojua unabii hukumu ilianza mwaka 1844 B.K. mbinguni, mwisho wa miaka 2300 ya Danieli 8:13,14 iliyoanza 457 K.K. Hukumu imejengwa juu ya Amri Kumi. Kwa hiyo, kumcha Mungu ni kuishi kwazo. **"Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikia; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya" (Mhu.12:13,14; Soma pia Mt.12:30-37; 1Yoh.5:2,3; Ufu.14:12; 12:17).**

Malaika wa pili anatangaza anguko katika makanisa ya Kiprotestanti yaliyokuwa Marekani wakati ule ambayo yalikataa kuupokea ujumbe ule wa hukumu uliotangazwa kuanzia 1840 hadi 1844 na Vuvuvugu Kuu la Kiadventista lililoongozwa na William Miller. Kanisa mama lilikuwa tayari limeanguka au limekengeuka mbali na kweli ya Biblia tangu karne ya tatu. **"Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanywesha mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake" (Ufu.14:8).** Mume wa Kanisa ni Kristo; hivyo kanisa likitafuta mume mwingine linazini. Linaacha

mafundisho ya Kristo, linafuata mafundisho yake potofu (Isa.4:1). Mafundisho hayo potofu huitwa “mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake”. Linganisha mafundisho ya kanisa lako na Biblia, utauona ukengeufu hapa na pale. Hali hiyo anaichukia sana Mungu. “Babeli” maana yake “machafuko” (Mwanzo 11:1-9). Mfano rahisi: Ubatizo. Wengine wanazamisha majini, wengine wanamwagilia maji kichwani, wengine wananyunyiza maji kichwani, wengine wanapita chini ya bendera, wengine wanaruka moto, na kadhalika. Je! hayo si machafuko au Babeli? Mungu wetu si Mungu wa machafuko (1Kor.14:33). Watu wote wanatakiwa warudi na kufuata mafundisho ya Biblia, Neno la Kweli (Yn.17:17).Wasingoje anguko kubwa la mwisho(Mt.7:24-27;Lk.6:46-49;Ufu.18 na 19).

Malaika wa tatu anatoa onyo kali sana. Chapa au alama ya Mnyama [Mfalme – Dan.7:17,23] ni siku ya Jumapili, siku ya kwanza ya juma (Lk.24:1-12). “Muhuri au alama ya Mungu ni Sabato ya siku ya saba ya juma, yaani, Jumamosi (Kut.20:8-11; Isa.8:16; Eze.20:12,20; 9:3-11; Ufu.7:1-4;Rum.4:11). Siku hizi mbili zitaleta mgogoro wa mwisho mbaya sana duniani utakaofuatiwa na mapigo saba ya Ufunuo 16 kwa walio sugu. Dunia nzima yapaswa kulizingatia onyo hilo maana mgogoro huo hauko mbali kuanzia sasa.

**“Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama [mfalme] na sanamu yake, na kuipokea chapa [Jumapili] katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganya na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo. Na maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku, hao wamsujuduo huyo mnyama na sanamu yake, na kila apokeaye chapa ya jina lake” (Ufu.14:9-11; soma Ufu.13:15-17). “Mvinyo ya ghadhabu ya Mungu” ni mapigo saba ya Ufunuo 16 (Ufu.15:1; 16:1,2).**

Hasira ya Mwana-Kondoo itatimizwa atakapokuja (Ufu.6:14-17). Kiburi cha mwanadamu kitashushwa chini (Isa.2:11-22). Tokeni Babeli (Ufu.18:1-8). Je, utasimama pamoja na kundi la watakatifu, “hao wazishikao amri za Mungu na Imani ya Yesu” (Ufu.14:12) au utakuwa katika kundi la waasi litakalotimua mbio ajapo? Fikiria sana, amua leo. Licha ya mateso watu wa Mungu watashinda vibaya sana (Ufu.12:11; 15:2,3).

Mfululizo na.17#mm

[TOA FOTOKOPI, MGAWIE MWENZAKO]

## UJUMBE WA MALAIKA WATATU

Kabla Mungu hajaleta maangamizi yake juu ya wanadamu waasi au kufanya jambo lo lote dhidi yao anawajulisha manabii ili watoe onyo kwao wapate kujirekebisha. **“Hakika Bwana MUNGU hawezi kufanya neno lo lote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake” (Amosi 3:7; Soma pia Yer.18:7-10; Mwanzo Sura ya 6 na 7; 18 na 19; Yona 3:1 hadi 4:1).** Kipindi hiki tunachoishi kinafanana na kile cha Nuhu na cha Sodoma na Gomora (Mt.24:37-41; Luka 17:26-37). Siku ile Yesu anapokuja na mawingu wataonekana tai wakila maiti za waasi (Mathayo 24:26-28; Ufunuo 19:11-21; Yer.25:32-37). Hiyo si habari njema!
Mwanadamu amejifanya ana hekima kuliko Mungu. Mambo aliyoyaweka Mungu, yeye anayageuza apendavyo ili yakidhi matakwa yake. Jaribio la kutisha mno ni lile la kubadili Amri Kumi za Mungu (Kut.20:3-17; Dan.7:25; 2 The.2:1-12). Hilo limeifanya dunia yote itende dhambi bila kujua. “Dhambi ni uvunjaji wa Sheria ya Amri Kumi” (1 Yoh.3:4 AJKK; Rum.7:7; 5:12,13; 4:15; 3:20; Yak.2:10-12). Na la pili ni kupaangusha patakatifu chini kwa kuwafanya wanadamu wawaangalie viongozi wa dini na kuungama dhambi kwao badala ya kupeleka maungamo yao kwa Kristo,

Kuhani Mkuu, katika Hekalu la Mbinguni
(Ebr.4:14-16); na la tatu ni kuiangusha